

UFANISI WA HUDUMA ZA UZAZI WA MPANGO: NYENZO YA KUBORESHA AFYA YA MAMA NA MTOTO

Uhakika wa Kupata Dawa na Vifaa Utaongeza Ufanisi wa Huduma

Tanzania ni mojawapo ya nchi ambazo zina viwango vya juu vya vifo vya Watoto na Wanawake kutokana na Uzazi. Kutokana na hali hiyo, Tanzania ina malengo ya kupunguza kiwango cha vifo vya Wanawake kutoka 454 kwa kila vizazi hai 100,000 kwa mwaka 2010 hadi vifo 193 ifikapo mwaka 2015; na kiwango cha vifo vya watoto walio chini ya umri wa miaka mitano kutoka vifo 81 kwa kila vizazi hai 1,000 kwa mwaka 2010 hadi vifo 54 ifikapo mwaka 2015. Ili kufikia malengo hayo, upatikanaji wa huduma za uzazi wa mpango kwa uhakika ni muhimu.

Fedha Zinapochelewa Kutolewa Huathiri Ufanisi wa Huduma

Tanzania ina lengo la kuongeza matumizi ya njia za uzazi wa mpango kufikia 60% ifikapo mwaka 2015 kutoka 27% ya mwaka 2010. Wakati huo huo, 22% ya watu wanaohitaji huduma hizi hawazipati. Pia, kwa kuongeza matumizi ya huduma hizo inakadiriwa kwamba taifa litaepusha mimba milioni 1.4 zisizotarajiwa; visa milioni 1 vya utoaji mimba; vizazi milioni 2.9 visivyotarajiwa; vifo 18,000 vya wanawake vitokanavyo na uzazi; na vifo 500,000 vya watoto, ikiwa huduma za uzazi wa mpango zitapatikana kwa ufanisi. Hata hivyo, fedha zinazotengwa kila mwaka kwa ajili ya huduma za uzazi wa mpango hazikidhi mahitaji halisi ya gharama za huduma hizo. Zaidi ya hilo, fedha zinazotolewa hazitoki kwa wakati muafaka na hutolewa kidogo kidogo, hivyo kuathiri upatikanaji wa huduma kutokana na kukosekana kwa vifaa na dawa za huduma hizo. Kushoto ni jedwali linaloonyesha namna ambavyo fedha zimekuwa zikitolewa kwa miaka nane iliyopita kati ya mwaka 2004/05 na 2011/12. Ili kutimiza malengo ya taifa ni muhimu kuhakikisha kwamba huduma hizo zinapatikana kwa wale wanaozihitaji zaidi kwa kutoa fedha za huduma hizo kwa ufanisi.

Mwaka wa MTEF	Kasma iliyokisiwa	Kasma iliyotengwa	Fedha iliyotoka	Uwiano na makisio
2004/05	7.7 bn	7.7 bn	7.7 bn	100
2005/06	6.9 bn	6.9 bn	6.9 bn	100
2006/07	6.9 bn	4.8 bn	8.7 bn	126
2007/08	6.4 bn	4.3 bn	2.2 bn	34
2008/09	9.2 bn	3.4 bn	5.0 bn	54
2009/10	9.6 bn	3.5 bn	7.5 bn	78
2010/11	24.0 bn	3.5 bn	14.6 bn	61
2011/12	20.0 bn	5.2 bn	4.0 bn	20

Kuongeza Ufanisi wa Kutoa Fedha Kutaboresha Huduma

Utoaji wa fedha za huduma za uzazi wa mpango huathiriwa na mambo mbalimbali yakiwemo kasi ndogo ya ukusanyaji wa mapato ya serikali, wingi wa vipaumbele vya serikali, utashi mdogo wa kisiasa, urasimu unaochukua muda mrefu katika taratibu za serikali, na sababu za kiuchumi. Matokeo yake, vituo vingi vya huduma hukosa dawa na vifaa vya kutolea huduma za uzazi wa mpango na kusababisha watumiaji kulazimika kukatisha huduma hizo. Wakati mwingine, kutokana na kutegemea ufadhili wa wahisani na ucheleweshaji wa kutoa fedha hizo, serikali huidhinisha mafungu makubwa ya fedha ifikapo mwishoni mwa mwaka wakati ambapo huduma zimeshachelewa kuwafikia wanaozihitaji. Ni muhimu kuangalia namna nyingine za kutatua matatizo haya. Matumizi ya mfumo wa Dhamana ya Ahadi (Pledge Guarantee) pamoja na kuruhusu Asasi za Kiraia (AZAKI) kupata dawa na vifaa hivi moja kwa moja kutoka kwenye Bohari Kuu ya Madawa (MSD) ni kati ya njia zinazoweza kuongeza ufanisi wa utoaji wa huduma hizi.

Dhamana ya Ahadi ni mfumo wa kuiwezesha serikali kupata dawa na vifaa vya huduma kwa wakati muafaka kwa kufanya makubaliano na wauzaji ili malipo yatolewe mwishoni mwa mwaka wakati ambapo fedha hupatikana. Kwa kutumia mfumo huu, serikali hutumia ahadi za wahisani pamoja Dhamana ya Ahadi kama mkataba wa malipo husika pasipo kutozwa riba yoyote.

Mapendekezo ya Kisera

- Serikali ikubali kutumia Dhamana ya Ahadi kuhakikisha kwamba wananchi wanapata huduma kwa wakati
- Serikali iruhusu AZAKI kushiriki kwenye mchakato wa kukadiria mahitaji ya huduma za uzazi wa mpango
- Serikali iruhusu AZAKI kupata dawa na vifaa vya huduma za uzazi wa mpango moja kwa moja kutoka MSD

Rejea

- i. Mpango wa Kitaifa Uliokasimiwa wa Utekelezaji wa Huduma za Uzazi wa Mpango. 2010 - 2015 (NFPCIP). Dar es Salaam, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii (Machi, 2010).
- ii. Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania II (MKUKUTA II). Wizara ya Fedha na Uchumi. (Julai, 2010)
- iii. Kibassa, B. and Muwonge, M. (Juni, 2012). Technical Assistance Report. Access to Contraceptive by CSOs and Public Sector Contraceptive Finance Tracking.

Kwa taarifa zaidi wasiliana na:
Health and Development Tanzania
P.O.Box 65147
Dar Es Salaam
Email: advocacy@hdt.or.tz

